

جمعية الدعوة والإرشاد وتنمية المجالس بالزلفي
مشروع تعلم الإسلام - ما هو الإسلام - اللغة السواحلية

Somo la 3

الدرس الثالث

MTUME MUHAMMAD- REHEMA NA AMANI ZA ALLAH ZIWE JUU YAKE:

Kwa hakika Allah amemtuma Muhammad - Rehema na Amani Za Allah ziwe juu yake -akamfanya yeye kuwa mtume wa mwisho na akaufanya ujumbe wake kuwa ujumbe wa mwisho.

Allah amemtuma mtume Muhammad - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake - ili awaongoze watu kumuabudu Allah peke yake na kuacha kumuabudu asiekua Allah kama Masanamu, Mizimu na vinginevyo. Amepewa utume Muhammad -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- akiwa na umri wa miaka Arobaini katika mji mtukufu wa Makkah.

Na alikua mtume Muhammad- Rehema na amani za Allah ziwe juu yake -ni mwenye kusifika na tabia njema katika jamii yake, kama vile ukweli, uaminifu, adabu za hali ya juu, mpaka jamaa zake wakampa jina na kummuita Muaminifu.

Alikua hasomi wala haandiki (Ummiyu), Allah akamfunulia Qur-an tukufu ambayo wameshindwa kuileta mfano wake viumbe vyote.

MISINGI YA DINI YA KIISLAM

1- Kumuamini Allah: Hii ni asili ya dini ya kiislam, na ndio Imani ya kumuamini Allah, na kumsadikisha kwa uwepo wake, na kwamba Allah ndio muumba wa kila kitu na yeye peke yake ndio mwenye kuupangilia ulimwengu wote, naye ndio anaestahiki kuabudiwa bila ya kushirikishwa na yeote, na yakwamba Allah ni mwenye kusifika na kila sifa ya ukamilifu na ametakasika na kila aina ya aibu na mapungufu, na kwamba hafanani na kiumbe yeote yule.

2- Kuamini Malaika: Malaika ni ulimwengu wa ghaib (visivyo onekana) wameumbwa kwa kutekeleza Ibada tu, hawahusiki na mambo ya uumbaji wala kuabudiwa.Na muislam anatakiwa kuamini kuwepo kwao, na kwamba malaika wako wengi, hakuna anaejua idadi yao isipokuwa Allah tu.

3- Kuviamini Vitabu: Muislamu anatakiwa aamini yakwamba Allah –Aletakasika na mapungufu-ameteremsha vitabu kwa baadhi ya Mitume na Manabii wake, kwa lengo la kubainisha haki na kuilingania, Mfano: Taurati kwa Nabii Mussa, Injili kwa Nabii Issa, Zaburi kwa Nabii Daudi, na kuiamini Qur-ani ambayo Allah aliiteremsha kwa Mtume wake wa mwisho Muhammad -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake-.

Qur-an: Huu ni ujumbe wa Allah alioutuma mwisho kwa ajili ya wanaadamu, na Allah hatokubali matendo ya mmoja wenu isipokuwa kwa kufuata kilichokuja ndani ya Qur-an, na Qur-an hii imekuja kutia nguvu Vitabu vilivyotangulia na kuvisadikisha, pia kinapambanuka kitabu hiki yakwamba Allah ameahidi kukihifadhi na kukilinda, hakiingii dosari wala mabadiliko, hii inaenda tofauti na Vitabu vilivyotangulia, ambavyo vilibadilishwa, ni kwa sababu tu kwamba Allah hakuahidi kuvilinda na kuvihifadhi kama ilivyo kwenye Qur-an.

4- Kuwaamini mitume: Muislam anatakiwa kuamini yakwamba Allah aliwatuma kwa lengo la kuwaambia wanaadamu kuwa wamuabudu yeye peke yake, na kukiacha kila kinachokwenda kinyume na hilo.

Na kwamba Mitume ni wanaadamu walioumbwa na wala hawahusiki kwenye uumbaji wala kuabudiwa, sifa yao ni kuwa binaadamu wa kawaada ambao wanakula, kunywa, kuugua, na kufa.

Mitume ni viumbe bora ambao Allah aliwachagua na akawahuisha wao tu kuwapa ujumbe.

Kuwaamini mitume ni pamoja na kuamini walichokuja nacho kutoka kwa Allah kuwa ni kweli, pamoja na kuamini majina yao kwa wale tuliofundishwa kwa majina, na kusadikisha maelezo yao kisha kuifanyia kazi sheria na muongozo uliokuja na wa mwisho wao Muhammad -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- kwani Allah hakubali sheria ya Mtume mwingine yeote yule.

5- Kuamini siku ya mwisho: Nayo ni siku ya Qiyaama, ambapo Allah atawafufua watu wote kwa ajili ya kuhesabiwa na kulipwa, imeitwa siku ya mwisho kwakuwa hakutakuwa na siku nyingine baada ya hiyo, hapo ndipo watu wa peponi watakaa majumbani mwao na watu wa motoni nao watakaa majumbani mwao.

6- Kuamini Qadari: Hii ni kuamini mwanaadamu kwamba Allah anajua kilichopo kilichopita na kitachokuja, na akitakacho Allah kitakuwa na asicho kitaka hakiwezi kutokea, na kwamba hakitoeki chochote kile ila kwa elimu yake (anakijua) na utashi wake.